


# WIZARA YA UJENZI



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## TAARIFA KUHUSU BODI YA MFUKO WA BARABARA TANZANIA

MEI 2014

# YALIYOMO

<b>1.</b>	CHIMBUKO LA MFUKO WA BARABABA .....	2
<b>2.</b>	VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO .....	3
2.1.	Vyanzo vya mapato .....	3
2.2.	Matumizi ya fedha za Mfuko .....	3
<b>3.</b>	MUUNDO WA BODI YA MFUKO WA BARABARA. ....	4
<b>4.</b>	MAJUKUMU NA KAZI ZA BODI YA MFUKO WA BARABARA. ....	9
4.1.	Dira na Maarubu ya Bodi .....	9
4.2.	Malengo ya Bodi. ....	9
4.3.	MAJUKUMU YA BODI YA MFUKO WA BARABARA .....	9
<b>5.</b>	UTENDAJI KAZI WA BODI YA MFUKO WA BARABARA. ....	10
5.1.	Makusanyo ya Mfuko.....	10
5.2.	Mgao wa Fedha za Mfuko.....	10
5.3.	Ripoti ya utendaji ya Mwaka.....	12
<b>6.</b>	MAFANIKIO YALIYOFIKIWA TOKA KUENZISHWA KWA BODI.....	13
6.1.	Kukua kwa Mfuko .....	13
6.2.	Kuboreka kwa Mtandao wa barabara.....	15
6.3.	Kukidhi Bajeti .....	15
6.4.	Kuimarika kwa Matumizi ya Mfuko .....	16
<b>7.</b>	CHANGAMOTO ZILIZOJITokeza.....	17
<b>8.</b>	MIKAKATI NA MALENGO YA BODI KWA MIAKA IJAYO. ....	18
8.1.	Kuongeza ukubwa wa mfuko. ....	18
8.2.	Kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi.....	19
8.3.	Kuongeza juhudi katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato.....	19
8.4.	Kuongeza uwezo wa kutumia fedha za mfuko. ....	19
8.5.	Kuongeza ufanisi .....	20
8.6.	Mapendekezo ya kuboresha Sheria ya Mfuko wa Barabara. ....	20

## **1. CHIMBUKO LA MFUKO WA BARABABA**

Bodi ya Mfuko wa Barabara ikiwa ni moja ya matunda ya Uhuru wa Tanzania Bara yaliyofikiwa chini ya Wizara ya Ujenzi ilianzishwa mwaka 2000 ikiwa ni moja ya mikakati ya Wizara ya Ujenzi katika kuboresha sera za taifa katika Sekta kuu ya barabara hususani katika mfumo wa kutoa fedha za matengenezo ya barabara.

Ili kuwezesha mabadiliko haya yaanze, Serikali ilitunga Sheria ya ushuru wa Barabara (Marekebisho) (Na.2) ya 1998, iliyopitishwa na Bunge tarehe 11 Novemba 1998 na kuhalalisha kuundwa kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Barabara. Rais aliyekuwepo madarakani kipindi hicho aliridhia Sheria hiyo tarehe 23 Desemba 1998.

Bodi ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa chini ya Sheria hiyo iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2006, na kuitwa " Road and Fuel Tolls Act Cap 220, Revised edition 2006" kwa ajili ya kuusimamia Mfuko wa Barabara.

Majukumu ya Bodi kwa mujibu wa Sheria ya Tozo za Barabara kwa muhtasari ni pamoja na yafuatavyo;

- Kuhakikisha kunakuwepo na ukusanyaji mzuri na upelekaji wa makusanyo ya ushuru wa barabara kwenye akaunti ya Mfuko,
- Kuishauri Serikali kuhusu vyanzo vipya vya ushuru wa barabara ikiwa ni pamoja na marekebisho ya viwango vilivyopo vya ushuru,
- Kutoa fedha kwa wakala ikiwa ni pamoja na TANROADS, Serikali za Mitaa na wakala nyingine za barabara na kufuatilia matumizi yake.

Mfuko wa Barabara umeundwa hususani kwa ajili ya kutoa fedha za matengenezo ya barabara kwa upande wa Tanzania bara kwa kuhakikisha mtiririko endelevu wa fedha ili kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara. Mfuko wa barabara unawaunganisha watumiaji wa barabara na Wakala wa Barabara kwa kuhakikisha huduma nzuri ya matengenezo ya barabara.

## **2. VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO**

### **2.1. Vyanzo vya mapato.**

Vyanzo vya mapato kwa mujibu wa sheria ni:

- (i). Ushuru wa barabara unaotozwa katika mafuta ya petroli na dizeli
- (ii). Ushuru wa magari ya kigeni mipakani
- (iii). Tozo ya magari yaliyozidisha uzito (hiki hakichukuliwi kama chanzo halisi cha mapato)
- (iv). Pamoja na chanzo kingine chochote katika kiwango au viwango vitakavyoamuliwa na Bunge mara kwa mara.

### **2.2. Matumizi ya fedha za Mfuko**

Kufuatana na Sheria hii Mfuko wa barabara umeanzishwa kwa masharti yafuatayo:

- (i). Fedha zote zinazokusanywa kama ushuru wa barabara zitawekwa katika akaunti ya Mfuko huu.
- (ii). Angalau asilimia isiyopungua tisini ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara zilizoainishwa pamoja na gharama za kiutawala zinazohusiana na shughuli hizo katika Tanzania Bara kulingana na mipango ya utendaji iliyoidhinishwa ambayo imepangwa na:
  - a) TANROADS kwa upande wa barabara kuu na barabara za mikoa; na
  - b) Mamlaka za Halmashauri kwa upande wa barabara za wilaya na miji, kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.
- (iii). Asilimia isiyozidi kumi ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa uendelezaji barabara pamoja na gharama za kiutawala katika Tanzania Bara kwa kufuata mipango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

## a) UFUNGUZI WA DARAJA LA MWANHUNZI



Ufunguzi wa Daraja la Mwanhunzi lililofunguliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete

### 3. MUUNDO WA BODI YA MFUKO WA BARABARA.

Bodi ya Mfuko inaundwa na jumla ya wajumbe tisa ikichanganya wajumbe toka Serikalini na wale wa Sekta Binafsi wakiwakilisha Watumiaji wa barabara kupitia kwenye vyama mbalimbali. Wajumbe wa sasa wa Bodi ni kama ifuatavyo:


S/N	JINA	UTEUZI	ASASI ANAYOIWAKILISHA
1.	Dkt James Wanyancha	Mwenyekiti	Sekta Binafsi
2.	Inj. Musa I Iyombe	Mjumbe	Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi
3.	Bw. Jumanne A. Sagini	Mjumbe	Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
4.	Dkt. Servacius Likwelile	Mjumbe	Katibu Mkuu Wizara ya Fedha
5.	Inj. Ven Ndyamukama	Mjumbe	Mkurugenzi wa barabara , Wizara

<b>S/N</b>	<b>JINA</b>	<b>UTEUZI</b>	<b>ASASI ANAYOIWAKILISHA</b>
			Ujenzi
6.	Bw. Willigis .O. Mbogoro	Mjumbe	Muungano wa Washirika Tanzania
7.	Bw. Leopold B Kabendera	Mjumbe	Chama cha Waendeshaji Utalii Tanzania
8.	Bw. Fulgence Bube	Mjumbe	Chama cha Wasafirishaji Tanzania
9.	Inj. Peter D. Chisawillo	Mjumbe	Chama cha Wafanya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania

## **b) PICHA ZA WAJUMBE WA BODI YA MFUKO WA BARABARA**




Dr. James Mnanka Wanyancha  
Chairman



Eng. Musa Iyombe  
Permanent Secretary  
Ministry of Works



Mr. Leopold B. Kabendera  
Representing Association of  
Tour Operators



Dr. Servacios Likwelile  
Permanent Secretary  
Ministry of Finance



Mr Jumanne Sagini  
Permanent Secretary  
PMORALG



Eng. Ven Ndyamukama  
Director of Rural Roads - MoW



Mr. Peter D. Chisawillo  
Representing Tanzania  
Chamber of Commerce,  
Industries and Agriculture



Mr. Fulgence Bube  
Representing Truck Owners  
Association



Mr. Willigis O.Mbogoro  
Representing Confederation  
of Co-operatives




Mr. Joseph O. Haule  
S Secretary

Watendaji wakuu wa shughuli za Bodi ya Mfuko ni Sekretariati inayoongozwa na Meneja wa Mfuko wa Barabara anayesaidiwa na Idara kuu tatu. Kwa sasa Sekretariati ina jumla ya wafanyakazi kumi na nne. Meneja wa Mfuko wa barabara ni Ndugu Joseph Haule.



Kwa ufupi muundo wa Bodi ya Mfuko ni kama unavyoonekana hapo chini:



## **4. MAJUKUMU NA KAZI ZA BODI YA MFUKO WA BARABARA.**

### **4.1. Maono na na Dhima ya Bodi**

#### **4.1.1. Maono**

Kuwa Taasisi ya mfano katika kutoa fedha za kugharimia matengenezo ya barabara nchini Tanzania.

#### **4.1.2 Dhima**

Kugharamia kwa ukamilifu na umadhubuti fedha za ujenzi wa barabara na kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha hizo katika ujenzi wa barabara kadri utakavyofanywa na Wakala wa ujenzi wa barabara hizo.

### **4.2. Malengo ya Bodi.**

Malengo ya Bodi ni haya yafuatayo:

- (1) Kutoa fedha za kutosha,
- (2) Kuhakikisha upelekaji fedha kwa uthabiti na kwa wakati.
- (3) Kuhakikisha kuwa fedha zinatumiwa vizuri ili watumiaji barabara waone thamani ya fedha zao.
- (4) Kuongeza uelewa miongoni mwa watumiaji barabara juu ya matokeo ya kiuchumi ya kuwa na barabara nzuri.

### **4.3. MAJUKUMU YA BODI YA MFUKO WA BARABARA**

Majukumu ya Bodi kama yalivyoainishwa katika Sheria iliyoitunda ni pamoja na:

- Kumshauri Waziri kuhusu vyanzo vipya vya ushuru wa barabara, marekebisho ya viwango vilivyopo vya ushuru na kuhusu kanuni za ukusanyaji wa ushuru wa barabara kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwepo kwa mtiririko wa kutosha na wa uhakika wa fedha kwa ajili ya shughuli za barabara,
- Kuhakikisha kunakuwepo na ukusanyaji mzuri na upelekaji wa makusanyo ya ushuru wa barabara kwenye Akaunti ya Mfuko;

- Kutoa fedha kutoka kwenye Mfuko kupeleka TANROADS (wakala wa Barabara ya Taifa Tanzania), Serikali za mitaa na wakala nyingine za barabara;
- Kuhakikisha kuwa shughuli za TANROADS, Serikali za Mitaa na Wakala nyingine za barabara na Mfuko zina ufanisi mzuri wa kimahesabu na kiufundi;
- Kufuatilia matumizi ya fedha zilizopelekwa TANROADS, Serikali za Mitaa na wakala nyingine za barabara kwa madhumuni ya malengo ya Mfuko;
- Kutoa mapendekezo mengine yoyote kwa waziri wa Barabara yatakayoonekana ni muhimu ili kuiwezesha Bodi kutimiza madhumuni yake

## **5. UTENDAJI KAZI WA BODI YA MFUKO WA BARABARA.**

### **5.1. Makusanyo ya Mfuko.**

Mapato ya Mfuko wa kwa sasa yanakusanywa kwa kupitia Mamlaka ya kodi ya mapato (TRA) kabla ya kupelekwa Hazina kwa tozo ya mafuta na Magari yanayopita mpakani na baadae kuhamishiwa kwenye akaunti ya Bodi ya Mfuko wa barabara kwa ajili ya kugawa kwa Mawakala wa barabara. TANROADS inakusanya mapato ya tozo ya Magari yanayozidisha uzito.


### **5.2. Mgao wa Fedha za Mfuko.**

Sheria iliyounda Bodi ya Mfuko wa barabara inaitaka Bodi kuingia mikataba ya utendaji na Mtendaji Mkuu wa TANROADS au Wakala nyingine inayopewa fedha na Mfuko. Bodi pia inatakiwa kuwasilisha taarifa ya mwaka kwa Waziri anayehusika na Barabara katika kipindi cha miezi mitatu, baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha kulingana na shughuli zake na za asasi zilizopewa fedha. Vigezo vinavyotumika kugawa fedha za mfuko ni;

- Urefu wa barabara
- Hali ya barabara ,na

- Aina ya barabara husika.

Mfuko wa Barabara unagawiwa kwa watumiaji kama ifuatavyo:



### 5.3 Ufuatiliaji wa Fedha za Mfuko

Baada ya Mgao wa Fedha kufanyika kwa kiungia kwenye mikataba ya utendaji kazi na Mawakala wa barabara (performance Agreement) ufuatiliaji wa matumizi ya Fedha za mfuko ili kuhakikisha thamani halisi ya matumizi ya Fedha(value for Money) unafanywa kwa njia zifutazo:

- i).Kwa kuwataka mawakala kuleta ripoti za utendaji na matumizi ya Fedha kila robo ya Mwaka.
- ii).Bodi kutembelea na kuona kazi za matengenezo ya barabara katika sehemu mbalimbali(Monitoring visits)
- iii).Kufanya ukaguzi wa kitaalam wa kazi za barabara(Technical audit) kwa kutumia Wahandisi washauri.

iv).Kutumia Wahandisi washauri walioko maeneo ya karibu kufuatilia kazi za barabara zinazoendelea.

v)Pia ukaguzi wa mahesabu na kazi unafanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kila mwisho wa mwaka wa Fedha.



Mwenyekiti wa Bodi Dkt James M. Wanyancha (katikati) akipata maelezo toka kwa Meneja wa TANROADS Iringa (Kushoto) juu ya matengenezo ya Barabara ya TANZAM – eneo la Kitonga. Kulia kwake Mwenyekiti ni Inj. Rashid Kalimbaga na kushoto kwake ni Bw. Kukwe Nyabusalo wa Bodi ya Mfuko wa Barabara)

vi) Ripoti ya utendaji ya Mwaka.

Kila mwishoni mwa mwaka wa fedha Bodi ya Mfuko wa Barabara inaanda taarifa ya utendaji ya Mwaka husika ikijumuisha utendaji wa Bodi na Mawakala wa Barabara na kuiwakilisha kwa Waziri anayehusika na shughuli za barabara kwa kuiwakilisha Bungeni kama Sheria iliyoanzisha Bodi inavyotaka.

## 5.4 Bajeti ya Mfuko kwa mwaka 2014/15


Maoteo ya bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 ni kama ifuatavyo;( katika shilingi bilioni za Kitanzania)

<b>Bajeti</b>	<b>Shilingi Bln</b>
<b>Mapato: Tozo ya mafuta</b>	
Mgao kwa Taasisi	751.7
TANROADS	469.5
TAMISEMI	223.6
Wizara ya Ujenzi	52.2
Bodi ya Mfuko wa Barabara	6.4

## 6. MAFANIKIO YALIYOFIKIWA TOKA KUENZISHWA KWA BODI

### 6.1. *Kukua kwa Mfuko*

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita hadi kufikia mwezi Juni 2012/13 Mfuko umekuwa kwa asilimia 75 (kutoka Shilingi bilioni 255.6 katika mwaka 2008/9 hadi Shilingi bilioni 447.8 katika mwaka 2012/13, kama inavyoonekana katika chati hapo chini.




Ukuaji huu wa mapato umewezesha ongezeko katika mgao wa fedha za matengenezo ya barabara kama ifuatavyo.

**Mgao wa Fedha za Mfuko toka mwaka 2008/9 hadi 2012/ 2013.**

Mwaka	2008/9	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13
Migao: T shs Bln	255.6	287.1	287.7	335.9	356.8

Katika kipindi hicho cha miaka mitano iliopita hadi kufikia Juni 2013, migao imepanda toka shilingi bilioni 255.6 mwaka 2008/9 hadi shilingi bilioni 356.8, mwaka 2012/13 kama inavyooneshwa katika chati hii hapa chini.




## 6.2. Kuboreka kwa Mtandao wa barabara

Hali ya Mtandao wa barabara umeboreshwa kwa kiwango kikubwa tangu Asasi zianze kupata fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Hali ya barabara zilizo katika hali nzuri na wastani kwa upande wa barabara Kuu na za Mikoa ilishuka kidogo toka kiwango cha asilimia 89 mwaka 2009/10 hadi asilimia 86 mwaka 2012/13. Hali ya barabara za Mijini, Mjazio na Wilaya iliongezeka toka asilimia 56 mwaka 2009/10 hadi asilimia 60 mwaka 2012/13.

Hali hii inafafanuliwa vizuri katika chati hii hapo chini:




## 6.3. Kukidhi Bajeti za matengenezo ya barabara

Mfuko umeweza kukidhi bajeti za matengenezo ya barabara kwa kila mwaka husika kwa kipindi chote cha miaka kumi na tatu tangu kuanzishwa kwake.

Jedwali hapo chini linaonyesha jinsi bajeti na migao ilivyokua kwa kipindi cha miaka mitano hadi kufikia mwezi Juni, 2013.





#### 6.4. Kuimarika kwa Matumizi ya Mfuko

Hali ya kupata hati safi ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa serikali kutokana na matumizi ya fedha za Mfuko ilikuwa ikiongezeka kwa kadri miaka ilivyokuwa ikiendelea kutokana na hatua mbalimbali zilizokuwa zikichukuliwa na Bodi kurekebisha hali nzuri ya matumizi ya mfuko kama inavyojionyesha katika jedwali la hapo chini:


TAASISI	FY 2005/ 06	FY 2006/ 07	FY 2007/08	FY 2008/ 09	FY 2009/10	FY 2010/11	FY 2011/12
<b>Bodi ya Mfuko wa Barabara</b>	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi
<b>TAMISEMI</b>	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi /chafu kwa baadhi ya Taasisi	Hati safi /chafu kwa baadhi ya Taasisi	Hati safi /chafu kwa baadhi ya Taasisi
<b>TANROADS</b>	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati chafu	Hati safi yenye hoja kadhaa
<b>Wizara ya Ujenzi</b>	Hati chafu	Hati chafu	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi	Hati safi

## 7. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

Pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu Bodi ilikabiliana na changamoto zifuatazo:

### i) Fedha kutotosha

Ingawa Makusanyo ya Mfuko yamekuwa yakiongezeka, fedha zimekuwa hazikidhi mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara. Kwa mfano kwa sasa fedha za Mfuko wa barabara zinakidhi asilimia sitini na nane ya mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa. Kama inavyoonekana katika kielelezo na chati hapo chini



### ii) Malimbikizo ya Matengenezo.

Kuna malimbikizo makubwa ya zamani ya matengenezo ya mtandao wa barabara uliosababisha barabara nyingi kuwa mbaya. Inakadiriwa kuwa kwa hivi sasa malimbikizo ya matengenezo yanakisiwa kuwa shilingi bilioni 1,035.24 kwa barabara Kuu na za Mikoa na shilingi bilioni 1,306.42 kwa barabara za Mijini, Mjazio na Wilaya.

**iii) Mtandao wa Barabara usioimarika.**

Karibu kiasi cha asilimia 93 cha mtandao ni Barabara za udongo, hivyo zinakuwa zikiharibika sana na kwa haraka wakati wa mvua kubwa na kupelekea fedha za mfuko kutumika katika matengenezo ya dharura.

**iv) Uzidishaji wa mizigo kwa watumiaji wa barabara**

Uzidishaji mizigo umeendelea kuwa tatizo pamoja na juhudi zinazofanywa kukabiliana nalo. Mpaka sasa kiasi cha asilimia 23 ya magari yanayopimwa yanakuwa yamezidisha uzito. Hali hii hufanya barabara zetu zichakae haraka kuliko uwezo wa Mfuko kugharamia matengenezo yake.

**v) Matumizi ya Fedha za Mfuko**

Mawakala wa barabara wamekuwa wanapata hati safi za ukaguzi wa hesabu toka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa serikali na hati safi toka kwa Wakaguzi wa Kiufundi. Hata hivyo bado kuna maeneo yanayohitaji maboresho zaidi kama vile matumizi mazuri ya pesa za mfuko ili kupata thamani halisi ya fedha zilizotumika na kuimarisha usimamizi wa mikataba ya kazi za matengenezo.

**vi) Kupanda kwa gharama za ujenzi na kushuka kwa thamani ya fedha ya Tanzania.**

Ingawa Fedha zimekuwa zikiongezeka kila mwaka lakini pia gharama za ujenzi zimekuwa zikipanda kwa kasi. Pia thamani ya fedha ya Tanzania imekuwa ikishuka mara kwa mara kutokana na sababu za kiuchumi. Hii inapelekea kupata matokeo madogo kwa fedha nyingi zilizopagwa kutumika katika matengenezo ya Barabara.

**8. MIKAKATI NA MALENGO YA BODI KWA MIAKA IJAYO.**

**8.1. Kuongeza ukubwa wa mfuko.**

Bodi inategemea kuongeza mfuko kwa kiasi kikubwa kwa kupanua wigo ili kuweza kukidhi mahitaji yote ya matengenezo ya barabara. Bodi itaendelea kupendekeza kwa Serikali vyanzo mbalimbali vya

mapato yakiwemo yale yanayotokana na vyanzo vinavyohusiana na matumizi ya barabara kama vile:

- a). Ada za Ukaguzi wa magari
- b). Ushuru wa magari makubwa ya mizigo
- c) Tozo ya gesi asilia mafuta ya mimea katika gari
- d). Matumizi ya Hifadhi ya barabara
- c). Kiasi kidogo cha michango ya Bima za magari.

### **8.2. *Kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi.***

Bodi imeandaa mwongozo unaoelezea pamoja na mambo mengine hatua za kuchukuliwa kwa wale watakaotumia kinyume na taratibu fedha za Mfuko. Mwongozo huo utaanza kutumika baada ya kupita ngazi husika.

Vilevile Bodi imeanza kuwatumia Wahandisi ushauri (Technical Consultants) kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kiufundi na ubora wa kazi (Technical and value for money audit) wakati miradi ya matengenezo ya barabara ikiwa inaendelea (preventive audits). Hii itawezesha kubaini na kurekebisha mapema mapungufu yoyote katika kazi za matengenezo ya barabara.

### **8.3. *Kuongeza juhudi katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato.***

Bodi itashirikiana na taasisi zingine kama vile Tanzania Revenue Authority (TRA), EWURA SUMATRA n.k katika hatua za kupunguza uvujaji wa mapato kama vile uchakachujaji wa mafuta, uuzaji wa mafuta yanayo kwenda nje ya nchi kwenye soko la ndani n.k.

### **8.4. *Kuongeza uwezo wa kutumia fedha za mfuko.***

Bodi itasimamia kikamilifu katika uwezo wa kutumia fedha za mfuko kwa Wakala wa Barabara kwa wakati uliopangiwa na kwa malengo yaliyokusudiwa.



Injinia R. Lwakatare wa Bodi ya Mfuko (wa pili kulia) akikagua ubora wa Kalvati kwenye Barabara ya Gulumungu-Shindai- Mwangiligili, Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

### **8.5. Kuongeza ufanisi**

Kuboresha ufanisi katika shughuli za kiutendaji za Bodi kwa kuongeza uwezo wa watendaji wa Sekretariati na mfumo wa utendaji.

### **8.6. Mapendekezo ya kuboresha Sheria ya Mfuko wa Barabara.**

Bodi imewasilisha mapendekezo ya kuiboresha sheria iliyoanzisha Bodi ili kutoa adhabu kali kwa watendaji wanaohusika na matumizi mabaya ya mfuko na kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za Bodi.